

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

04

HISABATI

Muda: Saa 1: 30

Mwaka: 2021.


Maelekezo


1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**

Katika swali la 1 – 5, kokotoa swali ulilopewa na kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi iliyotolewa.

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
1. (a)	Andika thamani ya tarakimu iliyopo nafasi ya nne kutoka kulia kwenda kushoto kwa namba 49051		
	(b) Andika 32 kwa namba za Kirumi		
	(c) Andika namba 76502 kwa kirefu		
	(d) Andika namba ifuatayo kwa kifupi: $2000 + 900 + 70 + 5$		
	(e) Andika namba 435 kwa maneno		
2. (a)	Jaza namba inayokosekana katika mpangilio wa namba ufuatao: 50, 40, 30, _____, 10		
	(b) Panga namba zifuatazo kuanzia kubwa kwenda ndogo: 23, 64, 32, 46, 29, 38, 54.		
	(c) Andika namba ya Kirumi inayofuata katika mpangilio ufuatao: V, XVI, XXVII, XXXVIII, _____.		

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu						
	(d) Urefu wa Mrisho, Samweli, Zalia na Rose uko katika mfululizo unaoongezeka kwa sm 12. Mrisho ana urefu was m 112, Samweli sm 124 na Zalia sm 136. Ikiwa Rose ni mrefu Zaidi, je, ana urefu wa sentimeta ngapi?								
	(e) Kadeu alifikiria namba. Alipata namba inayofuata kwa kujumlisha 5 kwenye namba iliyotangulia. Ikiwa namba ya kwanza ya kwanza aliyofikiria ni 20, namba ya tano katika mpangilio huo itakuwa ngapi?								
3.	(a) Jumlisha; <table style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <tr> <td>Saa</td> <td>dakika</td> </tr> <tr> <td>14</td> <td>30</td> </tr> <tr> <td>+ 8</td> <td><u>40</u></td> </tr> </table>	Saa	dakika	14	30	+ 8	<u>40</u>		
Saa	dakika								
14	30								
+ 8	<u>40</u>								
	(b) Shule ya msingi Azimio ina wavulana 340 na wasichana 318. Je, kuna jumla ya wanafunzi wangapi?								
	(c) Toa; <table style="margin-left: auto; margin-right: auto;"> <tr> <td>Saa</td> <td>dakika</td> </tr> <tr> <td>6</td> <td>45</td> </tr> <tr> <td>- 4</td> <td><u>50</u></td> </tr> </table>	Saa	dakika	6	45	- 4	<u>50</u>		
Saa	dakika								
6	45								
- 4	<u>50</u>								
	(d) Bahati alitembea kutoka nyumbani hadi sokoni kwa muda wa saa mbili. Je, muda huo ni sawa na dakika ngapi?								
	(e) Ronaldo alicheza mpira wa miguu kwa dakika 40 katika mchezo wa dakika 90. Je, hakuchenza dakika ngapi?								

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
4.	(a)	Chora umbo la pembe tatu sawa.		
	(b)	Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo: 		
	(c)	Mzingo wa pembetatu n ism 57. Ikiwa pande zote zinalingana, tafuta urefu wa upande mmoja.		
	(d)	Tafuta mzingo wa umbo la mraba lifuatalo: 		

Na.		Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
	(e)	Mzingo wa pembetatu ni sm 45. Ikiwa upande mmoja una urefu was m 12, upande wa pili sm 15, tafuta urefu wa upande wa tatu.		
5.	(a)	Tazama picha zifuatazo zinazowakilisha idadi ya wanafunzi katika Mikoa mitatu mwaka 2015, kisha jibu maswali yanayofuata.  Ufunguo: Kila picha nzima inawakilisha wanafunzi 50,000.		
	(a)	Je, Mikoa yote kwa pamoja ina wanafunzi wangapi?		
	(b)	Kuna jumla ya wanafunzi wangapi Iringa na Tanga?		
	(c)	Mkoa upi una wanafaunzi wachache zaidi?		
	(d)	Wanafunzi wa Tanga ni sehemu gani ya wanafunzi wote?		
	(e)	Kuna tofauti ya wanafunzi wangapi kati ya idadi kubwa Zaidi na idadi ndogo Zaidi ya wanafunzi?		